WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

HESLB
BODI YA MIKOPO
Investing in the Future



# MWONGOZO WA UTOAJI MIKOPO YA ELIMU KWA WANAFUNZI WA SHAHADA YA AWALI

2024/2025

Unapatikana:

www.moe.go.tz
www.heslb.go.tz
www.nactvet.go.tz

#WeweNdoFuture
#TimizaWajibu

HESLB Tanzania   HESLB_Tanzania   HESLBTanzania   info@heslb.go.tz

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **ACSEE** | Cheti cha Kidato cha Sita |
| **BS** | Vitabu na Viandikwa |
| **CLB** | Wanufaika wanaoendelea na masomo |
| **CSEE** | Cheti cha Kidato cha Nne |
| **FTCA** | Waombaji wa mkopo kwa mara ya kwanza wanaoendelea na masomo |
| **FPT** | Mafunzo kwa vitendo |
| **HESLB** | Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu |
| **MA** | Chakula na malazi |
| **MT** | King’amua uwezo |
| **NACTVET** | Baraza la Taifa la Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi |
| **OLAMS** | Mfumo wa maombi na usimamizi wa mikopo |
| **PDF** | Fomu ya ulemavu wa mzazi |
| **RES** | Gharama za utafiti |
| **RITA** | Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini |
| **SCSF** | Fomu ya Ufadhili |
| **SDF** | Fomu ya ulemavu ya mwombaji |
| **SES** | Hali ya kijamii na kiuchumi |
| **SIPA** | Akaunti ya kudumu ya mwanafunzi |
| **SFR** | Mahitaji Maalumu ya Kitivo |
| **TASAF** | Mfuko wa Maendeleo ya Jamii |
| **ZCSRA** | Wakala wa Matukio ya Kijamii Zanzibar |
| **SOCF** | Fomu Maalumu ya Kituo cha Kulea Watoto Yatima |

# 1.0 MAELEKEZO MUHIMU KWA WANAFUNZI WOTE WANAOOMBA MIKOPO

Waombaji wote wa mikopo ya elimu ya juu kwa mwaka wa masomo 2024/2025 wanafahamishwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

(i) Kusoma na kufuata taratibu za maombi katika Mwongozo wa mwaka wa masomo 2024/2025;

(ii) Kuhakikisha kuwa namba ya mtihani wa Kidato cha Nne atakayoitumia mwombaji iwe sawa kwenye maombi ya mkopo na udahili wa chuo;

(iii) Waombaji ambao wamefanya mtihani wa Kidato cha Nne zaidi ya mara moja wahakikishe wanaorodhesha namba zote za mtihani katika maombi yao;

(iv) Kuhakikisha kuwa nyaraka zote za maombi ya mkopo anazowasilisha mwombaji ziwe zimehakikiwa na mamlaka husika;

(v) Kuhakikisha kwamba vyeti vyote vya kuzaliwa/vifo vimethibitishwa na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) au Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar (ZCSRA) au Afisa aliyeteuliwa ili kuthibitisha uhalali wa nyaraka hizo;

(vi) Kuhakikisha wanafunzi waliozaliwa nje ya nchi au wanafunzi ambao wazazi wao wamefariki dunia wakiwa nje ya nchi wanaambatanisha barua za uthibitisho kutoka RITA au ZCSRA;

(vii) Waombaji wajaze fomu zao kwa ukamilifu na kuzisaini kabla ya kuziwasilisha HESLB kwa njia ya mtandao;

(viii) Kila mwombaji ahakikishe taarifa zake za benki zimejazwa kwa usahihi kwenye fomu ya maombi ya mkopo. Taarifa hizo ndizo zitakazotumika kumlipa mwanafunzi mkopo wake kipindi atakachokuwa masomoni, hivyo hazitaruhusiwa kubadilishwa bila HESLB kujulishwa rasmi;

(ix) Namba ya simu ya mkononi ya mwombaji itakayotumika wakati wa kusajili maombi ya mkopo ndiyo itakayotumika kumtaarifu hatua mbalimbali za maombi yake;

(x) Waombaji wote wanakumbushwa kuzingatia muda wa mwisho wa kutuma maombi kwa njia ya mtandao.

# 2.0 KWA UFUPI

Mwongozo huu ni kwa ajili ya wanafunzi ambao wanatarajia kuomba mkopo wa elimu ya juu kwa ajili ya kugharimiwa masomo ya Shahada ya Kwanza katika vyuo vya elimu ya juu ndani ya nchi kwa mwaka wa masomo **2024/2025.**

# 3.0 UHITAJI NA STAHIKI

Sheria na Kanuni za Bodi ya Mikopo zimeainisha sifa na vigezo vya jumla kwa wanafunzi wanaohitaji msaada wa kifedha wa kuzingatia sifa zifuatazo:-

### 3.1 Sifa za Jumla

(i) Awe Mtanzania mwenye umri usiozidi **miaka 35** wakati wa kuomba mkopo;

(ii) Awe amedahiliwa katika taasisi ya elimu ya juu Tanzania yenye ithibati;

(iii) Awe ameomba mkopo kupitia mfumo wa maombi ya mkopo **(OLAMS)**;

(iv) Asiwe na kipato kinachotokana na ajira au mkataba serikalini au sekta binafsi;

(v) Awe amerejesha angalau **asilimia 25** ya fedha za mkopo aliokuwa amekopeshwa awali. Hii itawahusu wanafunzi ambao waliacha au kuachishwa masomo;

(vi) Awe amehitimu elimu ya Kidato cha Sita **(ACSEE)** au Stashahada **(Diploma)** ndani ya miaka mitano, kati ya mwaka 2020 hadi 2024.

### 3.2 Sifa za Msingi kwa Wanafunzi wanufaika wanaoendelea na masomo (CLB) na wanafunzi wanaoendelea na masomo wanaoomba mkopo kwa mara ya kwanza (FTCA)

Pamoja na sifa zilizotajwa **3.1**, HESLB ina vigezo mahususi kwa wanufaika wa mkopo ambao wanaendelea na masomo kwa mwaka wa pili na kuendelea. Pia, kwa wanafunzi wanaoendelea na masomo ambao si wanufaika wa mikopo ya HESLB na wangependa kupatiwa mkopo:-

(i) Awe amefaulu mitihani kumwezesha kuendelea na mwaka wa masomo unaofuata;

(ii) Ikiwa anarejea masomoni baada ya kuahirisha, awe amepata barua ya kurejea masomoni (resumption letter) kutoka Taasisi ya elimu ya juu anakosoma;

(iii) Awe ni mnufaika wa mkopo ambaye hajarudia mwaka wa masomo kwa zaidi ya mara moja katika kipindi cha masomo yake;

(iv) Hatakiwi kuahirisha masomo kwa zaidi ya miaka miwili mfululizo katika kipindi cha masomo yake; na

(v) Anatakiwa kuwasilisha Namba ya Utambulisho ya Taifa **(NIN)** na namba ya usajili kabla ya kuwekewa fedha katika mwaka wa tatu wa masomo kupitia akaunti yake binafsi **(SIPA).**

## 4.0 NYARAKA ZA KUAMBATISHA KWENYE MAOMBI YA MKOPO

Zifuatazo ni nyaraka muhimu za kuambatisha kwenye maombi ya mkopo:-

(i) Cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na mamlaka husika, **ZCSRA** kwa waombaji waliozaliwa Zanzibar au **Namba ya Uthibitisho** (verification number) kutoka **RITA** kwa waombaji waliozaliwa Tanzania Bara;

(ii) Vyeti vya vifo kuthibitisha uyatima kutoka mamlaka husika, **ZCSRA** kwa mzazi/wazazi wa mnufaika waliofariki Zanzibar au **Namba ya Uthibitisho** kutoka **RITA** kwa mzazi/wazazi waliofariki Tanzania Bara

(iii) Fomu ya kuthibitisha Ulemavu wa mwombaji (**SDF-1)** iliyoidhinishwa na Mganga Mkuu wa Wilaya (**DMO**) au Mganga Mkuu wa Mkoa (**RMO**);

(iv) Fomu ya kuthibitisha Ulemavu wa mzazi wa mwombaji (**PDF-2**) iliyoidhinishwa na Mganga Mkuu wa Wilaya (**DMO**) au Mganga Mkuu wa Mkoa (**RMO**);

(v) Fomu ya udhamini (**SCSF-3**) ikiambatana na uthibitisho wa usaidizi wa

kifedha uliopokelewa na mwombaji katika ngazi ya elimu kabla ya chuo. Fomu ya **SCSF-3** iidhinishwe na Taasisi mdhamini wa mwombaji;

(vi) Namba ya mnufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (**TASAF**);

(vii) Fomu maalumu ya kituo cha kulelea watoto yatima (**SOCF**) kuanzia utotoni hadi hatua ya kudahiliwa katika chuo cha elimu ya juu.

(viii) Barua kutoka **RITA** au **ZCSRA** ili kuthibitisha taarifa za kuzaliwa kwa waombaji waliozaliwa nje ya nchi. Waombaji ambao mzazi/wazazi wao walifariki nje ya nchi wanapaswa pia kupata barua kutoka **RITA** au **ZCSRA** ili kuthibitisha taarifa iliyotolewa;

## 5.0 MASUALA YA KIPEKEE YA KUZINGATIWA

HESLB huzingatia makundi mbalimbali ya waombaji kwa lengo la kuhakikisha kunakuwa na uwiano sawa miongoni mwa waombaji na vipaumbele vya Taifa. Kutokana na hilo, upangaji wa mikopo utawapa kipaumbele waombaji kutoka makundi yaliyo chini kiuchumi na uzito wa programu utafuata kama inavyoonesha katika kipengele cha **6.0**.

Makundi hayo yatajumuisha; Yatima; Wazazi wasiojulikana (unknown parents); kaya zenye kipato duni zinazofadhiliwa na mifuko kama **TASAF** au taasisi za aina hiyo kwa ajili ya ufadhili wa masomo ya shule ya sekondari na ulemavu kwa mwombaji au mzazi wake.

## 6.0 MAKUNDI YA PROGRAMU ZA MASOMO

Shahada zote zenye ithibati zitagawanywa katika makundi makuu matatu zikiakisi vipaumbele vya Taifa kama vinavyoainishwa katika Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Ujuzi (NSDS) kama ifuatavyo:-

### 6.1 Programu za Kundi la Kwanza

**(i) Ualimu wa Sayansi:** (Fizikia, Kemia na Baiolojia), Ualimu wa Hisabati na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi;

**(ii) Sayansi za Afya:** Udaktari, Upasuaji Meno, Udaktari wa Wanyama, Ufamasia, Uuguzi, Ukunga, Shahada ya Sayansi katika Prosthetikia na Mifupa, Shahada ya Sayansi katika Mazoezi ya Viungo, Shahada ya Sayansi ya Afya na Maabara, Shahada ya Sayansi ya Maabara na Matibabu na Shahada ya Sayansi ya Teknolojia ya Mionzi;

**(iii) Programu za Uhandisi:** Ujenzi, Mitambo, Umeme, Uchimbaji Madini, Utengenezaji Nguo, Kemikali na Usindikaji, Kilimo, Chakula na Usindikaji, Magari, Viwanda, Usari Majini, Teknolojia ya Uhandisi wa Baharini, Elektroniki na Mawasiliano, Usindikaji na Huduma Baada ya Mavuno, Maji na Umwagiliaji, na Uhandisi wa Ndege;

(iv) Jiolojia ya Petroli, Kemia ya Petroli; Mafuta na Gesi;

(v) Kompyuta, Programu za Sayansi ya Kompyuta, Habari na Mitandao;

(vi) Takwimu Bima (Actuarial and Data Sciences);

(vii) Kilimo, Misitu, Sayansi ya Wanyama na Uzalishaji; na

(viii) Shahada ya Awali ya Sanaa katika Kiswahili; na

(ix) Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

### 6.2 Programu za Kundi la Pili

**(i) Programu za Msingi za Sayansi:** Shahada ya Sayansi ya Wanyama, Mimea, Kemia, Fizikia, Baiolojia, Baiolojia ya Viumbe Vidogo, Baiolojia ya Mifugo na Bioteknolojia, Uvuvi na Mifugo, Sayansi ya Mazingira na Uhifadhi, Jiolojia, Hisabati na Takwimu, Sayansi ya Mazingira na Usimamizi, Afya na Mazingira, Baioteknolojia na Maabara, Wanyamapori na Uhifadhi, Vipimo na Mizani.

**(ii) Programu ya Sayansi ya Ardhi:** Ubunifu Majengo, Ubunifu Mandhari nje ya Majengo, Usanifu Ndani ya Majengo, Uchumi Ujenzi, Mipango Miji na Vijiji, Usimamizi na Uthaminishi Ardhi, Teknolojia ya Jiospasho.

### 6.3 Programu za Kundi la Tatu

Sayansi za Jamii, Masomo ya Biashara na Uongozi, Uhasibu, Masoko, Fedha, Uchumi, Takwimu, Mazingira, Maendeleo ya Jamii, Ustawi wa Jamii, Masomo ya Maendeleo, Sosholojia, Sayansi ya Siasa, Sanaa, Uchoraji, Sayansi ya Ubunifu, Muziki, Sheria, Lugha, Fasihi, Jiografia, Saikolojia, Anthropolojia, Akiolojia na Masomo ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano.

Programu mpya zitakazopokelewa na HESLB zitajumuishwa katika kundi husika.

## 7.0 VIPENGELE NA VIWANGO VYA MIKOPO ITAKAYOPANGWA

### 7.1 Vipengele vya Mkopo na Viwango vya Juu vya Fedha

Waombaji watakaopangiwa mikopo watapangiwa viwango vya fedha kulingana na uhitaji wao. Kiasi cha jumla cha juu cha fedha kitagawanywa katika vipengele vya mkopo kwa mtiririko ufuatao: Chakula na Malazi (**MA**), Ada ya Mafunzo (**TF**), Gharama za Vitabu na Viandikwa (**BS**), Mahitaji Maalumu ya Kitivo (**SFR**), Gharama za Utafiti (**RES**) na mwisho Mafunzo kwa Vitendo (**FPT**).
HESLB itatoa mkopo kugharamia vipengele vyote au baadhi ya vipengele, kama ifuatavyo:-

#### 7.1.1 Chakula na Malazi (MA)

Kiwango cha juu cha **MA** kitakokotolewa kwa **TZS 10,000.00** kwa siku wakati wa mafunzo chuoni kulingana na kalenda ya chuo katika mwaka husika wa masomo.

#### 7.1.2 Viwango vya Ada ya Mafunzo (TU)

Kiwango cha juu cha ada ni **TZS 3,100,000.00** kwa mwaka kulingana na gharama zinazolipwa katika taasisi za umma za elimu ya juu.

#### 7.1.3 Gharama za Vitabu na Viandikwa (BS)

Kiwango cha juu cha **TZS 200,000.00** kwa mwaka kwa vitabu na viandikwa na kitatolewa kwa wanafunzi wahitaji wenye sifa.

#### 7.1.4 Mahitaji Maalumu ya Kitivo (SFR)

Kwa kuzingatia king'amua uwezo, mwombaji anaweza kupangiwa mkopo wa Mahitaji Maalumu ya Kitivo hadi asilimia mia moja **(100%)** kwa programu zenye mahitaji maalumu ya kitivo zilizoidhinishwa na TCU/NACTVET kwa kuzingatia viwango vilivyoidhinishwa kutumika katika vyuo vya umma.

**7.1.5 Mafunzo kwa Vitendo (FPT)**
Bodi itatoa kiasi cha **TZS 10,000.00** kwa siku hadi siku **56** kwa mwaka, kwa ajili ya Mafunzo kwa Vitendo. Mikopo kwa ajili ya Mafunzo kwa Vitendo itatolewa kwa programu zinazohitaji Mafunzo kwa Vitendo kama zitakavyopendekezwa na vyuo husika vya elimu ya juu na kuidhinishwa na Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET).

**7.1.6 Gharama za Utafiti (RES)**
HESLB inaweza kutoa hadi **TZS 500,000.00** kwa ajili ya kugharimia utafiti katika baadhi ya Programu za Sayansi ya Afya, Uhandisi, Kilimo na Sayansi ya Ardhi.

Programu nyingine za shahada ya kwanza zinaweza kupata mkopo kwa ajili ya utafiti kwa kiasi kisichozidi **TZS 100,000.00** katika mwaka wa mwisho wa masomo.

# 8.0 UTARATIBU WA MALIPO

Malipo ya Gharama za Chakula na Malazi, Vitabu na Viandikwa, Mahitaji Maalumu ya Kitivo, Mafunzo kwa Vitendo na Gharama za Utafiti zitalipwa moja kwa moja kwa mwanafunzi; wakati Ada ya Mafunzo italipwa moja kwa moja kwenye taasisi husika ya elimu ya juu. Malipo yote yatafanyika baada ya mnufaika kuthibitisha kwa njia itakayokuwa imeelekezwa na Taasisi husika ya elimu ya juu kupitia akaunti za benki zilizohakikiwa, ambazo ziliwasilishwa wakati wa kuomba mkopo.

Ikitokea mwanafunzi hajasaini kwa wakati, mkopo utarejeshwa HESLB baada ya **siku 30** kutoka tarehe ambayo taarifa ilifikishwa chuoni na mnufaika kutaarifiwa kuhusu malipo hayo kupitia simu yake ya mkononi. Kiasi KILICHOREJESHWA hakitalipwa tena kwa mwanafunzi na hakitakuwa sehemu ya deni lake. Malipo yoyote yatakayofuata lazima yathibitishwe na chuo.

# 9.0 MASHARTI MENGINE

**9.1 Wajibu Wa Wadhamini Na Wazazi**
Wazazi na wadhamini wana wajibu wa kuthibitisha usahihi wa taarifa ambazo zimewasilishwa katika fomu ya maombi ya mkopo kabla ya kusaini. Mdhamini wa mkopo anaweza kuwa mzazi, mlezi au ndugu au watu wanaokubalika kisheria kuwa mdhamini au mtu ambaye si Mwanafunzi mnufaika wa mkopo.
Wadhamini wanatakiwa kuhakikisha mikopo inarejeshwa na wanapaswa kufahamu mahali wakopaji walipo na ikitokea mnufaika akakwepa kulipa deni, mdhamini atalazimika kulipa mkopo huo.
Mwombaji wa mkopo anapaswa kuambatanisha picha (passport size) ya mdhamini

na nakala ya kitambulisho kimojawapo kati ya vifuatavyo, ambacho kimetolewa na mamlaka za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar:

(i) Kitambulisho cha Taifa
(ii) Kadi ya mpiga kura
(iii) Leseni ya udereva
(iv) Pasi ya kusafiria
(v) Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi

### 9.2 Urejeshaji wa Mkopo

Baada ya kuhitimu masomo ya elimu ya juu, mnufaika wa mkopo atatakiwa kurejesha mkopo wake wote kwa makato yasiyopungua asilimia kumi na tano **(15%)** ya mshahara wake wa kila mwezi au kiwango kisichopungua **TZS 100,000.00** kwa mwezi kwa mnufaika aliye kwenye sekta isiyo rasmi. Iwapo mnufaika ataachishwa/atakatisha masomo, mkopo huo wote utalipwa kwa mkupuo. Mikopo yote inatozwa asilimia moja (1%) ya ada ya uendeshaji kwenye deni la msingi la mnufaika kwa mara moja.

## 10.0 KUHAMA CHUO AU PROGRAMU NDANI YA CHUO

Endapo mnufaika wa mkopo atahama kutoka chuo kimoja na kwenda chuo kingine au programu moja kwenda nyingine ndani ya chuo alichodahiliwa, mkopo wake utahamishwa baada ya HESLB kupokea uthibitisho wa uhamisho wa mwanafunzi kutoka kwa mamlaka husika.

Uhamisho wa mkopo hautaathiri ongezeko la kiwango cha mkopo kilichopangwa awali isipokuwa tu pale ambapo mwanafunzi amehamishwa na mamlaka au itakavyoamuliwa na Bodi ya Mikopo.

## 11.0 JINSI YA KUOMBA MKOPO

Maombi yote ya mkopo yatafanyika kupitia Mfumo wa Maombi na Usimamizi wa Mikopo (OLAMS). Waombaji wote wa mikopo WANAKUMBUSHWA kutumia namba ileile ya Mtihani wa Kidato cha Nne iliyotumika wakati wa kuomba udahili.

Baada ya kukamilika kwa mchakato wa maombi kwenye mtandao, waombaji watapaswa kupakua (ku-print) nakala za fomu za maombi na Mkataba wa Mkopo kutoka kwenye mtandao, kugonga mihuri sehemu husika, kusaini fomu, kuambatisha nyaraka zinazohitajika na kuzipakia (upload) kwenye mfumo wa OLAMS kurasa zilizosainiwa

(namba 2 na 5).

# 12.0 ADA YA MAOMBI YA MKOPO

Waombaji wanapaswa kulipia ada ya maombi ya mkopo ya kiasi cha shilingi elfu thelathini **(TZS 30,000.00)** kwa namba ya kumbukumbu ya malipo wanayoipata katika mfumo na kulipia kupitia Benki au kwa mitandao ya simu. Kwa maelezo zaidi tembelea: https://olas.heslb.go.tz

# 13.0 TAREHE YA MWISHO YA MAOMBI YA MKOPO

Dirisha la maombi ya mkopo kwa mwaka **2024/2025** litafunguliwa tarehe **01, Juni, 2024** hadi tarehe **31 Agosti, 2024.** Mwongozo huu unapatikana kupitia www.heslb.go.tz

### 13.1 Orodha ya Waombaji waliopangiwa Mkopo

Orodha ya waombaji watakaopangiwa mikopo itatangazwa kupitia akaunti za kudumu za waombaji mikopo za SIPA**.**

# 14.0 RUFAA DHIDI YA KIWANGO CHA MKOPO

Waombaji ambao hawataridhika na viwango vya mikopo watakavyopangiwa wanaweza kukata rufaa kwa kujaza fomu za rufaa kwenye mtandao kupitia akaunti za kudumu za waombaji mikopo za SIPA**.** Dirisha la Rufaa kwa mwaka 2024/2025 litafunguliwa kuanzia tarehe **15 Septemba, 2024 hadi tarehe 30 Septemba, 2024**.

# 15.0 MAULIZO NA MALALAMIKO

Waombaji walio na maswali wanashauriwa kuwasiliana nasi kupitia Kituo cha Simu cha HESLB (0736 66 55 33); WhatsApp 0739 66 55 33 Mitandao ya Kijamii iliyothibitishwa yaani X, Instagram na Facebook (HESLB Tanzania) na e-Mrejesho (www.heslb.go.tz).
.

**Imetolewa na:-**
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**BODI YA MIKOPO YA WANAFUNZI WA ELIMU JUU**
**JUNI 1, 2024**

Call Centre +255 736 66 55 33
WhatsApp +255 739 66 55 33

HESLB Tanzania HESLB Tanzania HESLB_Tanzania

#Kazilendelee
#WeweNdoFuture
#TimizaWajibu

## DODOMA

PSSSF Building
Makole Road,
Uhundini.

P.O. Box 984,
Dodoma

+255 758 067577

+255 739 067577

info@heslb.go.tz

## DAR ES SALAAM

Higher Education
Students' Loans Board
1 Kilimo Street, Tazara,
Mandela Road
P.O. Box 76068,15471
Dar es Salaam
Phone: 0736 665 533
Email: info@heslb.go.tz

## ZANZIBAR

Michenzani Mall,
Michenzani Area
Fifth Floor
P.O. Box 900,Zanzibar,
Phone: 0779 321 424
Email: zanzibar@heslb.go.tz

## ARUSHA

NSSF Mafao House,
First Floor
P.O. Box 2712, Arusha
Phone: 027 2520128
0624 100 011
0739 102 016
Email: arusha@heslb.go.tz

## MWANZA

PSSSF Plaza, Second Floor
Kenyatta Road
P.O. Box 3051, mwanza
Phone: 028 2506008
0759 819 350
0738 153 661
Email: mwanza@heslb.go.tz

## MBEYA

CAG Building, Mbalizi Road
P.O. Box 319, Mbeya
Phone: 0738 131 310
0738 131 311
Email: mbeya@heslb.go.tz

## MTWARA

NHC Raha Leo Complex,
Second Floor
P.O. Box 969, Mtwara
Phone: 0733 068 171
Email: mtwara@heslb.go.tz